

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA NANE**

**KIKAO CHA NANE**

**04 FEBRUARI, 2015**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA NANE

KIKAO CHA NANE – TAREHE 04 FEBRUARI, 2015

#### I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

##### **MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:**

Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii katika kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari, 2015.

##### **MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii katika kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari, 2015.

## II. MASWALI:

### OFISI YA WAZIRI MKUU:

#### 83. MHESHIMIWA DKT. DAVID MCIWA MALLOLE (DODOMA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Serikali imefanya kazi nzuri ya kutengeneza barabara za Dodoma Mjini kupitia Fedha za Mfuko wa *World Bank* Awamu ya Kwanza:-

Je, ni lini fedha za Awamu ya Pili za *World Bank* zitatoka ili kukamilisha ujenzi wa barabara ambazo bado hazijawekewa lami katikati ya Mji wa Dodoma.

#### 84. MHESHIMIWA DEOGRATIAS ALOYS NTUKAMAZINA (NGARA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Watendaji wengi wa Vijiji na Kata wana uwezo mdogo sana kutokana na elimu duni waliyonayo na hawana fursa ya kujiendeleza kutokana na ufinyu wa bajeti na hivyo kuwa kikwazo cha maendeleo.

Je, ni lini Serikali itawaondoa Watendaji hao wenye uwezo mdogo na kuajiri Vijana wenye

elimu ya sekondari ambao wengi wao wapo huko vijijini (mtaani) baada ya kumaliza shule.

**85. MHESHIMIWA SAID MOHAMED MTANDA (MCHINGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, ni lini tatizo sugu la maji Mvuleni, Mnangole, Lihimilo na Kitohavi litapatiwa ufumbuzi na kwa gharama gani.

**WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

**86. MHESHIMIWA RITTA ENESPHER KABATI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Bunge lilipitisha sheria kwamba ajira zote za majeshi wachukuliwe vijana waliopitia JKT kama vile Jeshi la Magereza, Polisi nk:-

- (a) Je, mpaka sasa hivi ni vijana wangapi wameshanufaika na utaratibu huo;
- (b) Je, ni lini wafanyakazi walioko Serikalini ambao hawajapitia JKT na baadhi ya

Wabunge ambao hawajaenda JKT wataendelea na utaratibu huo.

**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

**87. MHESHIMIWA JOSEPH ROMAN SELASINI (ROMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi:- Shule zisizo za Serikali huweka Viwango Maalum na Tofauti vya Ufaulu kutoka kidato kimoja kwenda kingine:-

- (a) Je, Serikali inajua na kuunga mkono utaratibu huu hasa unapotumika kwa wanafunzi wa kidato cha tatu kwenda channe;
- (b) Je, kwa nini Serikali haiweki Kiwango elekezi kama utaratibu huo unakubalika;
- (c) Je, shule inapomrejsha au kumkataa mwanafunzi wa kidato cha tatu, huku sio kukwepa majukumu ya malezi, unyanyasaji wa kisaikolojia na kuzingatia biashara zaidi kuliko kutoa elimu.

## **WIZARAYA UCHUKUZI:**

### **88. MHESHIMIWA DKT. MARY MACHUCHE MWANJELWA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-  
Kiwanja cha Ndege kipya cha Kimataifa  
Songwe kimekamilika na kiko umbali wa km.  
25 toka Jiji la Mbeya:-

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kutumia  
Uwanja wa Ndege wa zamani kwa matumizi  
chanya kama vile hoteli kubwa.

## **WIZARA YA NISHATI NA MADINI:**

### **89. MHESHIMIWA KIDAWA HAMID SALEH (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na  
Madini:- Nchi yetu imebarikiwa utajiri mwingi  
wa Madini na Vito vya aina mbalimbali ikiwemo  
TANZANITE ambayo haipatikani mahali  
popote duniani isipokuwa Mererani – Arusha:-

(a) Je, ni kiasi gani cha mapato yatokanayo na  
mauzo ya Tanzanite kimepatikana katika  
Taifa kwa miaka 2011/2012, 2012/13 na  
2013/14;

(b) Je, ni kiasi gani cha mapato kimepotea kutokana na Vito vya TANZANITE kwa kuuzwa kwa njia isiyo halali katika kipindi cha miaka ya 2011 – 2014;

(c) Je, ni nani wanunuzi wakubwa wa TANZANITE Duniani.

**90. MHESHIMIWA MARIAM NASSOR KISANGI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini :- Serikali imeingia ubia na Mwekezaji katika eneo la TIPPER:-

(a) Je, Serikali imepata faida gani kutokana na uwekezaji huo;

(b) Je, kwa nini mpaka sasa hakuna uendelezaji mkubwa katika eneo la TIPPER;

(c) Je, ni lini uboreshaji wa mazingira ya TIPPER utakamilika.

## **WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:**

### **91. MHESHIMIWA AMINA MOHAMED MWIDAU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:- Utandawazi unaathiri kwa kiasi kikubwa utamaduni wa kila Taifa kwa sababu watu wengi wanajifunza kupitia mitandao mbalimbali kama Kompyuta, Smart phones na Televisheni:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kulinda utamaduni wetu.

## **WIZARA YA FEDHA:**

### **92. MHESHIMIWA CONCHESTA LEONCE RWAMLAZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:- Hadi sasa Serikali imekwishapokea takribani shilingi bilioni 15.5 kutoka Nchi ya Uganda kama fidia kutokana na uvamizi wa nchi hiyo wakati wa Vita ya Kagera ambayo iliathiri wakazi wa Mkoa wa Kagera:

Je, Wilaya ya Misenyi wamefidiwa kiasi gani.



## WIZARA YA KAZI NA AJIRA:

### 93. MHESHIMIWA RAJAB MBAROUK MOHAMED (OLE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Ajira:- Taasisi za fedha na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii hapa nchini, zimekuwa na fedha ambazo zimekaa muda mrefu bila kuchukuliwa na wenyewe kutokana na sababu mbalimbali, ambapo hazina huendelea kupeleka makato yao (**unclaimed assets**):-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani na fedha hizo;
- (b) Je, ni kiasi gani cha fedha hizo kipo mpaka sasa.

## WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

### 94. MHESHIMIWA HAMOUD ABUU JUMAA (KIBAHA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:- Kuna kero ya mashamba pori katika Jimbo la Kibaha Vijijini, kuna takribani mashamba themanini (80) ya Ngeta, Vikuge, Mpiji, Kikongo, Dutumi, Misufini, Mlandizi, Msongola, Kwala, Mperamumbi, Disunyara, Lupunga, Bokomnemela, Minazi Mikinda, Mkuza Mkwala,

Vikuruti na Soga ambayo yametumiwa ilani ya kufutiwa milki (*Notice of revocation*):-

Je, ni lini Serikali itayafutia milki mashamba hayo na kuirudisha ardhi hiyo kwa Wananchi.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI:**

### **95. MHESHIMIWA SHAFFIN AHMEDALI SUMAR (TABORA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Ajali za barabarani zimekuwa zikiongezeka siku hadi siku na kusababisha madhara mengi ikiwemo ulemavu na vifo:-

- Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka wazi taarifa na historia za madereva wote kwa kutumia vyombo kama tovuti ili kuwadhhibiti na kutathimini utendaji kazi wao kabla ya kuwaajiri kwani wengine hukimbia baada ya kupata ajali na kuajiriwa sehemu nyingine.

## **WIZARA YA MAJI:**

### **96. MHESHIMIWA KAPT. JOHN ZEFANIA CHILIGATI (MANYONI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Mradi wa Maji Mbwasa Wilayani Manyoni unaosambaza maji kwenye vijiji 10 vya Bonde la ufa uko kwenye Mpango wa Matokeo

makubwa sasa (BRN) na umetengewa fedha katika Bajeti ya mwaka 2014/2015:-

(a) Je, ni lini mradi huu utanza kutekelezwa na utachukua muda gani kukamilika;

(b) Je, mradi huo utagharimu kiasi gani cha fedha na hadi sasa Serikali imeshapeleka Manyoni fedha kiasi cha utekelezaji wa mradi huo.

**97. MHESHIMIWA JOSEPHAT SINKAMBA  
KANDEGE (KALAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-  
Upatikanaji wa maji katika Wilaya mpya ya Kalambo umekuwa wa tatizo kubwa sana ikizingatiwa kuwa mradi wa kuvipatia maji vijiji 10 kila Halmashauri unaofadhiliwa na Benki ya Dunia umechukua muda mrefu bila mafanikio:-

(a) Je, ni lini mradi huo utakamilisha usambazaji wa maji kwenye vijiji vya Mwazyee, Mwimbi, Kisumba na Matai;

(b) Je, ni lini vijiji vingine vyenye adha kubwa ya maji vya Myunga, na Kalalasi – Kata ya Mkali; Ulumi na Kalepula – Kata ya Kasanga; Ninga na Kafukula – Kata ya Katazi vitapatiwa maji;

(c) Halmashauri mpya ya Kalambo ilipata vijiji vitano tu badala ya vijiji 10; Je, ni lini Serikali itaongeza vijiji vingine vipya.

### **III. HOJA ZA KAMATI:**

#### **MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo kwenye Taarifa hiyo.

#### **MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo kwenye Taarifa hiyo.

#### **MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo kwenye Taarifa hiyo.

**DODOMA**

**DKT. T. D. KASHILILAH**

**04 FEBRUARI, 2015**

**KATIBU WA BUNGE**